JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA NNE

**8 SEPTEMBA, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 8 SEPTEMBA, 2017

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Miundombinu juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**39. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itakifanyia tathmini ya kina *(Ex-post evaluation)* Kituo cha Vijana cha TULU kilichopo Sikonge.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:-

**40. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Matatizo ya mipaka kati ya Hifadhi na Wanakijiji wanaopakana na maeneo ya Hifadhi ya Bwawa la Igombe katika Jimbo la Tabora Mjini ni ya muda mrefu hususan katika Kata za Kabila, Ikomwa na Misha:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro huo wa mipaka ambao ni wa muda mrefu.

**41. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Skimu ya Umwagiliaji ya Mng'aro imekuwa haina ufanisi mzuri tangu kuanzishwa kwake:-

(a) Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya Skimu hiyo ili kuleta tija;

(b) Je, ni lini Skimu hiyo itakaguliwa ili kuondoa malalamiko ya ubadhirifu wa mali za Ushirika.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**42. MHESHIMIWA MARTIN MTONDA MSUHA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

(a) Je, kuna Vituo vingapi vinavyorusha matangazo kwa njia ya Televisheni nchini na vinamilikiwa na Kampuni zipi;

(b) Je, ni Vituo vingapi vinarusha matangazo ya TV bure kwa Wananchi kupitia ving'amuzi.

**43. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Timu yetu ya Taifa imeendelea kufanya vibaya katika michezo ya Kimataifa:-

Je, Serikali imeliona hilo na imechukua hatua gani.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

**44. MHESHIMIWA WILLY QULWI QAMBALO (KARATU)**:-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Bei kubwa ya pembejeo hususan mbegu bora ya mahindi imesababisha Wakulima wengi kupanda mbegu zilizo chini ya kiwango na hivyo kusababisha uzalishaji hafifu sana, mfano msimu wa mwaka 2015/2016 kilo moja ya mbegu ya zao hilo iliuzwa kati ya shilingi 5000/= hadi 6000/=:-

(a) Je, ni nini kinafanya bei ya mbegu bora kuwa ghali sana;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wakulima wa zao hilo kupata mbegu hizo kwa gharama nafuu.

**45. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI)**:-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Ili kuboresha Kilimo na Ujasiriamali inahitajika elimu kwa Wakulima pamoja na kuwa na vyanzo vya mitaji:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Mfuko wa kuzunguka (*Revolving Fund*) kwa kila Kijiji kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Wakulima na Wajasiriamali;

(b) Je, Benki ya Wakulima ina mtaji kiasi gani na imetoa mikopo katika Mikoa gani;

(c) Je, ni lini Benki ya Wakulima itaanza kutoa mikopo kwa Wakulima wadogo wa Mbeya Vijijini.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-

**46. MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea nyumba Askari Polisi wa Pemba ili kuwaondolea adha ya makazi Askari hao.

**47. MHESHIMIWA ZUBEDA HASANI SAKURU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Hivi sasa kumekuwa na wimbi la

matukio ya ukamataji wa Wahamiaji haramu kwa wingi hapa nchini:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ongezeko la matukio hayo.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**48. MHESHIMIWA KAPT. (MST) GEORGE HURUMA MKUCHIKA (NEWALA MJINI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali ya Awamu ya Kwanza ilijenga Viwanda vikubwa viwili vya kubangua Korosho Newala Mjini kwa lengo la kuongeza thamani ya Korosho, kupanua ajira na kukuza uchumi; Viwanda hivyo vilibinafsishwa na mpaka sasa ni Kiwanda kimoja tu kinachofanya kazi kwa robo ya uwezo wake na kingine hakifanyi kazi kabisa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Viwanda hivyo vinafufuliwa na kufanya kazi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**49. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itajenga makazi bora katika Kituo cha Wazee cha Kolandoto kwa kuwa makazi haya yamekuwa ya muda mrefu na yamechakaa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**50. MHESHIMIWA MAFTAHA ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Manispaa ya Mtwara Mikindani ina migogoro mikubwa ya ardhi inayokaribia kusababisha uvunjivu wa amani:-

Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kutatua migogoro hiyo.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**51. MHESHIMIWA DKT. MARY MACHUCHE MWANJELWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, nini Sera ya Serikali katika *Shuttle Diplomacy* kwa kuzingatia mgogoro wa Ziwa Nyasa ambao umedumu kwa muda mrefu bila ufumbuzi pamoja na Historia yake ya *"Helgoland".*

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994, Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999, Itifaki ya Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004, Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008 na Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta duniani.

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**8 SEPTEMBA, 2017** — **KATIBU WA BUNGE**